Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU *Bulletin*

*JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.24 - 2022*

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaendelea kuboresha Elimu yetu*






# Vituo vyote vya OUT nchini kuunganishwa na Mkongo wa Taifa

- KAZI IENDELEE -




**BODI YA UHARIRI**

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
***Kamishna wa Elimu***

Atupele Mwambene
***Mkurugenzi wa Sera na Mipango***

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

Nelly Mtema
***Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Ipyana Mwaipaja

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## Nafasi ya kushiriki kuutengeneza Mfumo wa Elimu ipo na ni wajibu wetu kushiriki kwa pamoja

Yajayo katika Elimu yanafurahisha, huu ni Usemi ambao Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amekuwa akiutumia kila anapozungumzia maendeleo ya utekelezaji wa kazi ya Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 pamoja na mabadiliko ya Mitalaa.

Hii ni kuonyesha namna gani kazi hii muhimu kwa nchi inavyokwenda vizuri na kwa weledi katika kutuletea mfumo wa elimu ambao kila mmoja wetu atapata nafasi ya kujadili rasimu ya mapendekezo yatakayojadiliwa katika mjadala mkubwa wa kitaifa unaolenga kuhakikisha kila mwananchi katika nchi hii anashiriki katika mchakato wa kuweka mfumo wa elimu anaoutaka na anaouona unafaa kwa ajili ya watoto wa taifa hili.

Tulimsikia Prof. Mkenda katika mkutano wa wadau wa elimu uliofanyika jijini Dodoma akisema tayari zaidi ya maoni 100,000 yalikuwa yamepokelewa na kamati zinazoshughulikia mabadiliko ya mitaala na ile ya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Idadi hii kubwa ya wadau walioshiriki katika kutoa maoni na inatupa matumaini kuamini kwamba maoni yaliyotolewa ni mazuri na ndio maana tunamsikia Waziri akisema Yajayo yanafuraisha!

Hata hivi karibuni katika Mahafali ya 41 ya Chuo Kikuu Huria Jijini Mwanza, Prof Mkenda alisema ku na mambo makubwa ambayo yamependekezwa na wadau mbalimbali kwa kuwa utekelezaji wa kazi hiyo imeendelea kwa kushirikisha wadau mbalimbali na kupata uzoefu kutoka katika nchi zilizofanikiwa na zile ambazo hazijafanikiwa katika elimù.

Kongole kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutekeleza maagizo ya Mhe.Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi na ufanisi katika kuhakikisha mnatupatia mfumo wa elimu unaokwenda kumkomboa kijana wa Kitanzania na kumwezesha kushiriki katika uchumi wa taifa ama kimataifa kwa kujiajiri ama kuajiriwa katika soko la ajira la kimataifa.

Wito wangu kwa Watanzania wote ndani na nje ya nchi kuhakikisha muda wa mjadala wa kitaifa unapofika basi kila mmoja ashiriki katika kuutengeneza mfumo huu wa elimu tuitakayo na tusibaki nyuma kusubiri kulaumu ama kukosoa.

Uwekezaji katika TEHAMA >

# Vituo vyote vya OUT nchini kuunganishwa na Mkongo wa Taifa

- Bilioni 1.8 kujenga majengo mapya katika vituo vitano
- Maabara kujengwa katika mikoa saba





Wahitimu wa Vyuo Vikuu wameaswa kutumia vema elimu wanayopata kuleta tija kwa Taifa.

Hayo yamesemwa Jijini Mwanza na Mhe. Dkt. Phillip Mpango wakati wa mahafali ya 41 ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Aidha, Mhe. Mpango ameagiza Wizara ya Elimu kuhakikisha vituo vyote vya Chuo hicho vinaunganishwa na mkongo wa Taifa ili kuwezesha matumizi ya TEHAMA na kupunguza gharama za uendeshaji .

"Vituo vyote vya Chuo Kikuu Huria vitaunganishwa na mkongo wa Taifa na hili naagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha linafanyika mara moja ili kupunguza gharama za uendeshaji," ameongeza Mhe. Dkt. Mpango

Awali akiongea katika mahafali hayo, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia amesema Chuo Kikuu Huria kimetengewa fedha kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) kwa ajili ya ujenzi wa miundo mbinu, kusomesha wahadhiri na miradi mingine.

"Serikali kwa kutambua mchango wa Chuo Kikuu Huria katika kupeleka elimu kwa jamii kupitia mradi wa HEET tutajenga maabara saba katika mikoa ya Njombe, Arusha, Dodoma, Mwanza, Kigoma, Mtwara na Pwani ambazo zitajikita katika tafiti za kisayansi kulingana na shughuli na mahitaji muhimu ya eneo husika," amefafanua Waziri Mkenda.

Waziri Mkenda ameongeza kuwa Serikali imetoa zaidi ya Shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kujenga vituo vya Chuo Kikuu Huria katika mikoa ya Geita, Kigoma, Lindi, Simiyu na Manyara ambao mikoa hii ilikuwa ikitumia majengo ya kukodi kwa gharama kubwa.

Zaidi ya Wahitimu 4,000 wametunukiwa Shahada mbalimbali zikiwemo Shahada za Umahiri na Uzamivu wakiwemo wanafunzi kutoka nchi jirani za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Ghana, Malawi, Zambia, Congo, Namibia na Ethiopia.

Miundombinu ya Elimu >

# Serikali inakamilisha Ujenzi Chuo cha Ualimu Sumbawanga



Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa zaidi ya Shilingi bilioni saba kuwezesha ujenzi wa majengo mapya ya Chuo cha Ualimu Sumbawanga ambacho awali kilikuwa kwenye majengo ya kanisa Katoliki.

Akizungumza baada ya kuweka Jiwe la Msingi la ujenzi wa majengo hayo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa amesema fedha hizo zilikabidhiwa kwa Wizara ya Elimu ili isimamie ujenzi huo.

Ameongeza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kutoa fedha za kuboresha miundombinu ya elimu katika ngazi zote ili kuwezesha upatikanaji wa elimu bora inayoendana na mahitaji ya nchi.

"Serikali imetafuta fedha ya kujenga majengo haya katika kata ya Pito ili kukabidhi majengo ya awali kwa kanisa Katoliki, tunashukuru Manispaa ya Sumbawanga kwa kuweza kutoa eneo hili ili chuo kijengwe hapa," ameongeza Waziri Mkuu.

Aidha, Waziri Mkuu ameelekeza kufanyika uchunguzi wa Mhasibu wa chuo hicho pamoja na Katibu wa Kamati ya ujenzi wa mradi huo baada ya kukabiliwa na tuhuma za uchomaji moto nyaraka za ujenzi katika ofisi ya Mhasibu wa chuo.



Kwa upande wake Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga amemweleza Waziri Mkuu kuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amеridhia kiasi cha zaidi ya Shilingi bilioni 100 kutumika kwa ajili ya kujenga majengo mapya ya vyuo vya ualimu.

Mhe. Kipanga amevitaja baadhi ya vyuo hivyo kuwa ni Chuo cha Ualimu Ndala, Kabanga, Shinyanga, Dakawa, Muhonda na Sumbawanga ambavyo kuna vilivyokamilika huku vingine vikiendelea na ujenzi.

Kufuatia tuhuma za uchomaji moto ofisi ya Mhasibu chuoni hapo, Naibu Waziri amevunja Kamati zote za ujenzi wa Chuo hicho na kuagiza kuundwa kwa Kamati nyingine mara moja.

Ameongeza kuwa Serikali inamiliki vyuo 35 vya ualimu na kwamba vyuo 30 vimefanyiwa ukarabati mkubwa na kuongezewa miundombinu mipya ili kuhakikisha walimu wanatoa elimu bora katika mazingira bora.

Naye Mbunge wa Sumbawanga, Mhe. Aesh Hilaly ameishukuru Serikali kwa kujenga majengo hayo mapya ya chuo hicho, huku akiomba wasimamizi wa ujenzi kuhakikisha wanajenga majengo hayo kwa ubora.

Utekelezaji Mradi >

# Taasisi za Elimu ya Juu za Wizara ya Fedha zasaini utekelezaji Mradi wa HEET





Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa wito kwa Vyuo vya Elimu ya Juu vinavyotekeleza Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) kuhakikisha vinatekeleza azma ya Serikali ya kuwapatia vijana ujuzi, maarifa na stadi zitakazowawezesha kujiajiri ama kuajiriwa.

Wito huo umetolewa Jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Francis Michael wakati wa hafla ya utiaji saini wa makubaliano ya ruzuku ya Mradi wa HEET kwa Taasisi za Elimu ya Juu zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Kiongozi huyo amesema mradi huo unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika mawanda ya elimu ya juu nchini kwa kuwaandaa vijana watakaokuwa na uwezo wa kushindana katika soko la ajira la ndani na kimataifa kwa kujiajiri ama kuajiriwa.

"Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Benki ya Dunia wanataka kuona mradi huu ukiwaondoa vijana barabarani kwa kuwapatia ujuzi, maarifa na stadi zitakazowawezesha kujiajiri ama kuajiriwa, hivyo twendeni tukatekeleze mradi huu kwa mtazamo huo" amesisitiza Dkt Michael.

Katibu Mkuu huyo amezitaka Taasisi hizo kuhakikisha zinatekeleza mradi huo kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa, huku akisisitiza matumizi makini ya fedha.

Kwa upande wake Mratibu wa Mradi huo kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Amani Ngedu ameishukuru Wizara ya Elimu na Benki ya Dunia kwa kuzipatia Taasisi hizo mradi huo kwa kuwa unakuwa mradi wa kwanza mkubwa kwa taasisi hizo.

Ameongeza kuwa ushirikiano uliopo kati ya Wizara hizo mbili utasaidia katika kusimamia utekelezaji wa mradi huo katika taasisi hizo kwa ufanisi na weledi.

Taasisi za Elimu zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango zinazonufaika na Mradi huo ni Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Mipango (IRDP), Chuo cha Takwimu (EASTC), Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

# Mapendekezo Sera ya Elimu >



## 'Tupo tayari kwa mjadala wa Kitaifa kuhusu mapendekezo ya Sera ya Elimu na Mitaala'

Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu Msingi yamekamilika na yanasubiri mchakato wa ndani ya Serikali ili kupata ridhaa ya rasimu zilizoandaliwa kupelekwa kwa wadau kwa mjadala wa kitaifa.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Profesa Adolf Mkenda wakati akizungumza katika Mahafali ya 41 ya Chuo Kikuu Huria Jijini Mwanza, ambapo amesema kuna mambo makubwa ambayo yamependekezwa na wadau mbalimbali.

Prof. Mkenda amefafanua kuwa utekelezaji wa kazi hiyo umeendelea kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Maaskofu, Mashekhe, walimu, wamiliki wa shule binafsi pamoja na wataalamu kutoka nje ya nchi ili kupata uzoefu kutoka katika nchi zilizoleta mageuzi ya elimu na kufanikiwa na zile ambazo hazikufanikiwa.

"Tumekamilisha rasimu ya mapitio ya Sera, ina mapendekezo mengi makubwa, tunachosubiri sasa ni mchakato wa ndani wa kupitia mapendekezo hayo kabla hatujayatangaza rasmi kwa ajili ya mdahalo wa kitaifa na hatimae mchakato wa maamuzi uweze kufikiwa ndani ya Serikali," amesema Prof. Mkenda.

Akitolea mfano jambo moja ambalo limeguswa katika mapitio ya Sera ni suala la walimu kupewa kipaumbele katika ubora na suala la mafunzo endelevu kazini ambalo hata sasa suala hilo la mafunzo kazini limeshaanza na linaendelea.

"Katika mapitio ya Sera walimu waliopo wataendelea kupewa mafunzo kazini, ambayo tayari wameshaanza kuyapata na walimu wapya tutaona vigezo katika mapitio ya Sera kuhakikisha tunakuwa na walimu bora wa kuendeleza elimu yetu," amefafanua Prof. Mkenda.

Aliongeza kuwa kazi ya kupitia mitaala nayo inakwenda vizuri pamoja na kuwa kwa kawaida hapa nchini kazi hiyo ilikuwa haipelekwi katika ngazi ya maamuzi kutokana na kuwa ni kazi ya kitaalamu zaidi, lakini kwa mageuzi haya ya elimu italetwa kwenye ngazi za juu na kisha kujadiliwa na umma wa Watanzania.

Ameongeza kuwa mageuzi hayo ya mitaala yatafanyika pia katika ngazi ya Elimu ya Juu ambapo huko utaangaliwa zaidi ubora wa elimu.



# Utekelezaji Kueneza Kiswahili >






## Wizara yajizatiti kueneza kiswahili Afrika na kote Ulimwenguni

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imejizatiti kueneza lugha ya Kiswahili kwa kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili katika nchi za Afrika na ulimwenguni kwa ujumla.

Akizungumza jijini Dodoma wakati wa kukabidhi bango la Kiswahili kwa watumishi waliopanda Mlima Kilimanjaro kwa azma ya kusherehekea Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania kwa kubidhaisha lugha ya Kiswahili Kikanda na Kimataifa, Kaimu Katibu Mkuu Prof. James Mdoe amesema nia ni kuendeleza Kiswahili kwa kutoa mafunzo kwa watu wengi zaidi.

Amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeipa kipaumbele lugha ya Kiswahili kwa kuitangaza ndani na nje ya nchi ikitambua kuwa Uhuru wa Mwafrika upo katika kujikomboa kifikra, kiutashi, kiimani na kutokua na mipaka katika matumizi yake ya lugha ya Taifa.

"Kwa kutambua hilo sisi kama Wizara mama ya mafunzo nchini tunapoadhimisha Uhuru wa Mtanzania Kitaifa tuna fahari kubwa kuipa lugha ya Kiswahili hadhi yake kwa kuipandisha kileleni mwa Mlima Kilimanjaro kwa kauli mbiu "KISWAHILI KILELENI" na kuitangazia Dunia Uhuru wetu, na hamasa yetu ya kujikomboa kupitia lugha hii," amesema Prof. Mdoe

Aidha amesema kwa sasa lugha ya Kiswahili ina wazungumzaji takriban milioni 250 na kwamba lugha hiyo inafundishwa kwenye Vyuo Vikuu visivyopungua 150 duniani kote.

"Vyuo vya Tanzania vina makubaliano na vyuo vya nje kuendelea kufundisha Kiswahili, hata Wizara ina mikataba takribani minne na Wizara za Elimu za nchi nyingine kuhusiana na masuala ya kufundisha Kiswahili na bado tunaendelea na mazungumzo na nchi nyingine, lengo ni kukikuza Kiswahili," ameongeza Prof. Mdoe.

Naibu Katibu huyo ametumia muda huo kutoa wito kwa Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika mataifa mbalimbali kuendelea kuchochea matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mataifa hayo ikiwemo kufungua madarasa ya awali ya kufundisha Kiswahili.

"Nchini Malawi tayari tumefungua darasa la kufundisha lugha ya Kiswahili na imewezekana kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini humo ndio maana natoa wito kwa Mabalozi wengine kufanya hivyo ili kuendelea kukuza lugha yetu kimataifa," amefafanua Prof. Mdoe.

Naye Menna Yasser, aliyekuwa mgeni maalum katika tukio hilo ambaye pia ni mwalimu na mwandishi wa kitabu cha kwanza cha Kiswahili kutoka nchini Misri amesema anajivunia kujua lugha ya Kiswahili na kwamba ni vizuri Waafrika tukahifadhi utambulisho wetu na kujivunia kujua lugha ya Kiswahili.

"Tuongee na kuthamini lugha zetu badala ya kudhani kuzungumza lugha nyingine ndio ustaarabu," amesema Yasser.

Kwa upande wake Meja Mwinyikombo Ally ambaye ameghani shairi maalum la Kiswahili katika hafla hiyo amesema uhuru, heshima, umoja na utu uliopo baina ya Watanzania umeletwa na lugha ya Kiswahili kwani ndio ilikuwa nyenzo ya kuwaunganisha Watanzania na kupata uhuru hivyo kukiweka Kiswahili juu ya kilele cha Mlima Kilimanjaro ni kuashiria yale aliyokusudia Mwl. Julius Nyerere na jitihada za kuendelea kukibidhaisha Kiswahili.

Elimu Ujuzi >

# Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma kuchangia harakati za kuleta Elimu Ujuzi



Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma utaongeza nguvukazi yenye ujuzi na maarifa inayohitajika kwenye uzalishaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alipotembelea mradi wa ujenzi wa Chuo hicho katika eneo la Nala jijini Dodoma ikiwa ni moja ya miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa jijini hapa.

Amesema Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza kwa vitendo katika kufikia malengo ikiwemo ujenzi wa Chuo cha ufundi Dodoma ambacho kinakwenda kujibu hitaji la kuwa na wataalamu wenye ujuzi watakaotumika katika uzalishaji.

"Nampongeza Rais kwa maono makubwa aliyo nayo anasema uchumi unaotegemea viwanda anaweka muunganiko, anajenga vyuo ili kupata wataalamu hao, na nimefarijika kusikia Chuo hiki kitatoa fani ya maabara, hii itasaidia sana katika hospitali zetu,"amesema Mhe. Senyamule.

Mhe. Senyamule ametoa rai kwa Taasisi zinazotekeleza miradi jijini Dodoma kuhakikisha zinatunza mazingira kwa kupanda miti ili kutunza uoto wa asili na kupendezesha mazingira.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo amesema utekelezaji mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma ni juhudi za Serikali katika kuongeza ujuzi kwa vijana wa Kitanzania ili waweze kuutumia ujuzi huo katika soko la hapa nchini na kimataifa kwa kujiajiri na kuajiri wengine.

"Msisistizo wa Serikali yetu sasa ni elimu ujuzi, tunapitia mitaala ya shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ufundi na Vyuo vikuu. Hii ni kutokana na maelekezo ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaamini mitaala hiyo itakapokuwa tayari hata majengo yatakuwa tayari ili iweze kutumika kuzalisha ujuzi," amesema Naibu Katibu Mkuu Nombo.

Prof. Nombo ametoa rai kwa Watanzania kuuunga mkono juhudi za Serikali kwa kupeleka vijana kusoma katika Chuo hicho pindi majengo hayo yatakapokamilika ili waweze kupata ujuzi.

Naye Mshauri elekezi wa Chuo cha Ufundi Dodoma Mhandisi Aliki Nziku kutoka BICO amesema Chuo hicho kinajengwa kwa awamu mbili ambapo utekelezaji wa mradi awamu ya kwanza ulianza Juni 2021 na unatakiwa kukamilika Desemba 2022.

Amesema ujenzi unagharimu zaidi ya Shilingi bilioni saba na umefikia asilimia 75. Ameongeza kuwa awamu ya kwanza ya mradi ukikamilika Chuo kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 1,500 na awamu zote zikikamilika kitadahili wanafunzi 3,000.





# Weledi kwa Walimu >



## Walimu waaswa kupunguza matumizi ya viboko na vitisho kwa wanafunzi




Rai imetolewa kwa walimu wote wa shule za msingi,sekondari na vyuo nchini kupunguza matumizi ya viboko na vitisho kwa wanafunzi kama njia ya kufanya wafaulu katika masomo yao kwa kuwa huo si mtazamo sahihi.

Rai hiyo imetolewa Jijini Dar es Salaam na Kamishna wa Elimu, Dkt. Lyabwene Mtahabwa wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa siku mbili wa wadau wa Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu (TESP) ambapo alimwakilisha Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Francis Michael

Ameongeza kuwa walimu wanatakiwa wafahamu kuwa watoto wote hawana uwezo unaofanana hivyo wanatakiwa kuwachukulia watafute mbinu mbalimbali za kumsaidia kila mmoja.

"Maendeleo ya kweli katika nchi huletwa na elimu bora, elimu bora huletwa na walimu bora na walimu bora sifa yao kuu ni upendo kwa wanafunzi na wadau wengine wa elimu. Mwalimu ni kioo cha jamii, amejaa hekima na busara na ni kimbilio la watu wote," amesema Dkt. Mtahabwa.

Amesema lengo la mkutano huo ni kutafakari namna ambavyo mradi umekuwa ukitekelezwa na kujadili jinsi ya kuimarisha na kuendeleza mambo yaliyotekelezwa kwa mafanikio baada ya mradi kuisha.

"Kwa hiyo siku hizi mbili tutaangalia nini kimefanyika kupitia Mradi huu wa TESP na kisha kuweka mikakati ya namna ya kuendeleza mradi huu," ameongeza Dkt. Lyabwene.

Mratibu wa Mradi wa TESP, Cosmas Mahenge amesema mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Canada umejikita katika kuimarisha elimu ya ualimu, hasa katika ngazi ya Astashahada na Stashahada za Ualimu katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na kwamba una jumla ya zaidi ya Shilingi bilioni 90.

Ametaja kazi kubwa zilizofanywa na mradi huo kuwa ni kutoa mafunzo kwa Wakufunzi zaidi ya 1,300, kununua vifaa vya TEHAMA kwa vyuo vyote 35 vya umma na kuviunganisha katika mkongo wa taifa wa mtandao.

Nyingine ni ujenzi wa Chuo cha mfano cha Ualimu Kabanga, ujenzi na ukarabati katika vyuo saba, kukarabati na kujenga maktaba za kisasa, maabara za Tehama na za sayansi, kuimarisha uongozi kwa kuwapa mafunzo ya uongozi kwa viongozi na maafisa Wizara ya Elimu Makao Makuu lengo likiwa kuimarisha mfumo wa kusimamia elimu ya ualimu.

Pongezi kwa Waandishi >





# Wizara ya Elimu yatoa Tuzo kwa Waandishi wa Habari za Sekta ya Elimu



Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa tuzo kwa waandishi ambao wamekuwa wakiandika kwa umahiri habari za maendeleo ya sekta hiyo.

Tuzo hizo zimekabidhiwa jijini Dar es Salaam na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye wakati wa Kongamano la kwanza la Maendeleo ya Sekta ya Habari.

Waandishi waliokabidhiwa tuzo hizo ni pamoja na Kuringe Mongi kutoka Channel Ten, Mwamini Andrew kutoka TBC Taifa, Safina Yasir TBC One , Jacob Mosenda kutoka gazeti la The Citizen na Julius Okully kutoka Okully Blog.



Malengo ya Wizara >

# Wizara ya Elimu na Taasisi zake zakutana kutathmini malengo



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Francis Michael amezitaka Taasisi zilizo chini ya Wizara kukutana kila robo mwaka kufanya tathmini ya pamoja ya utekelezaji wa malengo.

Agizo hilo limetolewa Desemba 14, 2022 jijini Dar es Salaam katika kikao kati ya Wizara na Taasi zake kilicholenga kutathmini utekelezaji wa malengo ya robo mwaka mbili zinazoishia Desemba 2022.

"Kikao hiki kimetuleta pamoja Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambao ni watekelezaji wakuu wa miongozo, Sera na Mipango tunayojiwekea ili kufikia malengo yakiwemo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa na Ilani ya CCM", amesema Dkt. Francis Michael.

Katibu Mkuu ameongeza kuwa ameaona ni vema kuanzisha utaratibu wa kuwa na tathmini ya pamoja ili kutambua mafanikio ya malengo yetu, changamoto tunazokutana nazo ili kwa pamoja tuone wapi tuongeze kasi na kuweka uelekeo.

Amezitaka Taasisi pia kushirikisha wadau wakati wa kuandaa mipango ili kujua mahitaji halisi katika Sekta.

Amesema kwa kufanya hivyo itasaidia kuwa na mipango sahihi ya kutekeleza katika mwaka.

Katibu Mkuu Michael amepongeza Taasisi kwa kuendelea kutekeleza majukumu kwa ubunifu na kuwataka kuongeza kasi na kuja na mbinu za kibunifu zaidi ili kufikia malengo mapana ya kitaifa.

Katika hatua nyingine Dkt. Michael amewaagiza Taasisi kutangaza kazi kubwa zinazofanyika katika maeneo yao ya kazi kwani wananchi wana ari kubwa ya kusikia mafanikio hayo na si kujibu malalamiko tu.

"Fanyeni kazi na vyombo vya habari na tukifanya kitu kizuri tutangaze na kama kiongozi huwezi mwambie afisa habari aseme," ameeleza Dkt. Michael

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Abdul-Razaq Badru ameipongeza Wizara kwa kuja na mpango huo ambao amesema utasaidia katika kubadilishana uzoefu kutatua changamoto kwa pamoja na kupanga mikakati kwa pamoja kujenga timu ili kwa pamoja hatimae kufikia malengo mapana ya sekta.

Nae Dkt Mboni Ruzegea Mkurugenzi Mkuu wa Bodi Huduma za Maktaba amemshukuru Katibu Mkuu kwa hatua ya kuanzisha vikao hivi na kuahidi kuendelea kuimarisha mikakati ya kutangaza mafanikio na fursa mbalimbali zilizoko katika taasisi.





## NUKUU >

**"TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA"**

***– Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***
***Bungeni - April, 2021***

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifala Elimu ya Ufundi (NACTE),**
S.L.P 7109, DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz